BARAZA LA WAKUU WA SHULE ZA KIISLAMU TANZANIA

MTIHANI WA UTAMILIFU WA SHULE ZA KIISLAMU

KIDATO CHA NNE

ELIMU YA DINI YA KIISLAMU

MWONGOZO WA USAHIHISHAJI AGOSTI, 2026

1.

(i)	(ii)	(iii)	(iv)	(v)	(vi)	(vii)	(viii)	(ix)	(x)
B	D	D	A	E	A	C	E	D	C

Alama 01 @ swali = Alama 10

2.

ORODHA A	(i)	(ii)	(iii)	(iv)	(v)	(vi)
ORODHA B	D	G	F	A	C	E

Alama 01 @ swaliu = Alama 06

3. Faida atakazozipata mwenye kuwa na imani thabiti juu ya Malaika wa Allah (S.W).

(i) Atajiepusha na kumshirikisha Mwenyezi Mungu na viumbe wake hasa wale wasioonekana kama Malaika, Majini na kadhalika (Qur'an 37:149-154)

(ii) Atakuwa ni mwenye kufanya ibada kwa bidii na kujiepusha na maovu na machafu ili kupata cheo kama Malaika au zaidi.

(iii) Atakuwa ni mwenye kuepuka kufanya maovu popote alipo na muda wowote kwa kujua kuwa yupo pamoja na Malaika.

(iv) Mja anapoamini kuwa Malaika huandika na kuhudhurisha vitendo vyake kwa Mwenyezi Mungu, hufanya bidii katika kufanya mema zaidi na kuepuka maovu kadri ya uwezo wake.

(v) Muumini anapoamini kuwa Malaika humuombea maghfira kwa Mwenyezi Mungu, hufanya bidii katika kuzidisha mema na kuepuka maovu kadri awezavyo ili kupata msamaha wa Mwenyezi Mungu.

(vi) Atakuwa jasiri katika kupigania Uislamu maana atajua kuwa Malaika wa Mwenyezi Mungu wanamlinda kwa idhini yake.

Hoja 06 @ Alama 01 ½ JUMLA

Shulelibrary.com

4. Madhara ya kufuata kampeni za kudhibiti uzazi:

(i) Uhaba wa wafanyakazi, jamii ikishajiingiza katika kampeni za kuwataka watu wadhibiti uzazi basi mara nyingi matokeo yake huwa kinyume na makusudio ya sera. Wanajamii wakishaitikia wito watu huepuka mzigo wa kuzaa kwa hiyo baada ya jamii ikihitaji watu itakuwa vigumu kuirudisha jamii kwenye hali ya mwanzo.

(ii) Kuharibika kwa maadili ya jamii. Sera ya kudhibiti uzazi huathiri sana mwelekeo wa maadili katika jamii. Kuanza mwanaume na mwanamke wanakuwa na uhuru wa kufanya jimai na mtu yeyote. Hivyo hisia za uovu wa zinaa huondoka, hufikia hadi kiongozi kuwataka wazazi wawagawie watoto wao mipira ya kufanyia zinaa.

(iii) Kushindwa kuotokomeza zinaa. Tumeona baadhi ya madhara na hasara ambazo huweza kutokea pindi sera ya kudhibiti uzazi ikitkelezwa. Watu wengi haa miongoni mwa watetezi wa kampeni hii wanakiri.

(iv) Tishio la kuanguka kwa nguvu kazi ya Taifa. Iwapo idadi ya watu katika taifa itaendelea kupungua, kutokana na kudhibiti uzazi taifa litakuwa katika tishio la kupoteza nguvukazi kama itatokea janga lisilotazamiwa kama vita.

Hoja 03 @ alama 03 = JUMLA 09

5. Mambo ambayo akizingatiwa jamii itaishi kwa haki na uadilifu.

(i) Tawhid. Jamii ikizingatia kuwa wanadamu wote ni viumbed wa Mwenyezi Mungu mmoja asiye na mshirika, yeye pekee mwenye uwezo wa kujua zuri na baya, kujua ya sasa na yajayo na ameepukana na upungufu walionao viumbe ni msingi mkuu wa kupatikana kwa haki na uadilifu.

(ii) Utume (Risala). Kumpwekesha Mwenyezi Mungu hakunabudi kwenda sambamba na muongozo wake kupitia Mitume na vitabu vyake. Jamii ili iishi katika haki na uadilifu haina budi kuzingatia ujumbe wa Mitume na kwa zama hizi ni Mtume Muhammad (S.A.W).

(iii) Imani juu ya siku ya mwisho. Ujumbe wa Mitume umeambatana na taarifa juu ya hesabu ya mwisho. Kwa hiyo kuwepo siku ya mwisho ni motisha ya kumsukuma mtu kufanya matendo mema na kuepuka mabaya kwa kufanya uadilifu.

Hoja 03 @ Alama 03, JUMLA 09

6. Matumizi mengine ya Msikiti kwa kuhusianisha na Msikiti wa Mtume (S.A.W).

(i) Msikiti hutumika kama kituo cha kutolea elimu kwa jamii

(ii) Msikiti hutumika kama kituo cha mambo ya uchumni, kama ukusanyaji wa zakat na saqadat na kushauri waumini namna ya kujikwamua kiuchumi.

Shuleilibrary.com

(iii) Msikiti hutumika kwa mambo ya kijamii kama vile ndoa, mazishi na mikutano.(BUNGE)

(iv) Msikiti hutumika kama kituo cha kujihifadhi wasafiri waliofika katika eneo kwa mahitaji maalumu au wapita njia.(sufa)

(v) Msikiti hutumika kama kituo cha mambo ya kisheria, kupatanisha watu na kutatua migogoro.

(vi) Msikiti hutumika kujadili na kupanga mikakati ya maendeleo ya Uislamu.

(vii) Msikiti utumike kama kituo cha jeshi

Hoja 06 @ alama 01 ½ JUMLA 09

7. Mgawanyo wa makosa katika Uislamu.

(i) Makosa ya Hudud. Makosa ya Hudud ni yale ambayo yamekatazwa na Allah (S.W) na hukumu zake zimetajwa katika Qur'an au Sunnah. Mfano wa makosa hayo ni, kuritadi, uzinzi, wizi na ujambazi.

(ii) Makosa ya Qisas. Baada ya makosa ya Hudud kundi la pili ni makosa ya Qisas. Neno Qisas lina maana ya " Usawa" au " kufanana". Lina maana kuwa mt aliyetenda kosa Fulani ataadhibiwa vilevile na kwa namna ileile aliyotumia katika kumdhulumu mwenzake. Mfano makosa ya kuua.

(iii) Makosa ya Ta' azir. Ni makosa ambayo Qur'an na Sunnah haujaweka (wazi) adhabu Fulani maalumu. Adhabu za makosa ya aina hii hutolewa na Jaji kwa idhini ya kiongozi wa Kiislamu. Neno Taa'zir ya adhabu ambayo haijawekwa moja kwa moja katika Qur'an bali hutolewa na Jaji kwa kulinganisha kosa na adhabu na mazingira. Mfano, kutukana, kuiba mali ambayo haijafika nisaab, kukutwa mke na Mume ambao si maharimu ambao si maharimu wakiwa faragha.

Hoja 03 @ alama 03, JUMLA 09

8. Umar bin AbdulAziz aliitwa Khalifa wa tano kwa sababu zifuatazo:

(i) Alijenga mfumo wa maisha kwa misingi ya uadilfifu, haki na usawa.

(ii) Aliwaondoa magavana wote waliokuwa katili na jeuri kwa raia.

(iii) Alirejesha na kuimarisha Baitul-Mal ya Dola katika ukusanyaji na utumiaji wa rasilimali kwa uadilifu mpaka masikini wanaohitajia walikosekana.

(iv) Alitoa amri ya kusimamia marekebisho ya kipimo ili raia wasipunjwe katika kuuza na kununua.

Shulelibrary.com

(v) Alikuwa karibu sana na raia katika kutatua matatizo, kupokea na kufanyia kazi maoni juu ya uongozi wake

(vi) Hakutenganisha dini na serikali bali alisimamia kusimamisha swala, kutoa zakat na kuamrisha mema na kukataza maovu

(vii) Aliamuru askari wa Kiislamu kuchunga miiko ya vita iliyowekwa na Allah (S.W) na Mtume (S.A.W)

(viii) Aliandika waraka na kuusambaza nchi nzima ili kujenga udugu na mapenzi ya kweli baina ya raia wake na kundoa mishikamano ya kijahili.

Hoja 06 @ Alama 01 ½ , JUMLA 09

9. Ili wanaohiji waweze kufikia lengo la Hijjah zao yafuatayo yafanyike

(i) Kuhiji kwa chumo halali. Miongoni mwa sababu za kukubaliwa ibada ya hijjah ni kuhiji kwa chumo halali, kwa mujibu wa Hadith ya Mtume (S.A.W), Hijjah iliyohijiwa kwa gharama za chumo la haramu haitakjubaliwa. Hivyo kutopatikana kwa athari chanya kwa wanaohiji.

(ii) Kuchunga miiko ya hijjah. Ili athari njema ipatikane kwa anayehiji lazima achunge miiko yake ikiwemo na kujizuia kusema au kutenda machafu. Kwa hiyo mtu aliyekusudia kuhji ni lazima ajitahidi kuwa mcha Mungu ilia pate athari chanya ya ibada hiyo.

(iii) Kutekeleza nguzo za Hijjah vilivyo. Ibada ya Hijjah kama ibada nyingine imejengwa na nguzo zinazoipa sura yake halisi. Endapo nguzo za Hijjah hazitatekelezwa vilivyo, ima kwa kukusudia au kwa kutojua ibada ya hijjah haitaswihi, hivyo kutomfikisha hujaji kwenye athari chanya ya ibada hiyo.

(iv) Kuwa na elimu kuhusu lengo la Hijjah. Lengo la Hijjah kwa ufupi ni kuwatayarisha na kuwazoesha Waislamu kuwa Makhalifa wa Allah (S.W) hapa ulimwenguni. Kwa hiyo ukihiji bila kuwa na lengo hili akilini mwako huwezi kupata athari chanya ya Hijjah.

(v) Kujiepusha na Ria yaani kufanya kwa ajili ya Allah

Utanguli(i)zi **Alama 01 ½**

Kiini **Hoja 4@ alama 03 = 12**

Hitimisho **Alama 01 ½**

JUMLA ALAMA 15

10. Masharti ya matini ya Hadith sahihi:

Shulelibrary.com

(i) Isipingane na Qur'an

(ii) Isipingane na Hadith nyingine iliyothibitika kuwa ni sahihi

(iii) Isimzulie Mtume (S.A.W) kufanya jambo ambalo ni kinyume na Uislamu.

(iv) Isipingane na hakika (fact)

(v) Isiwe na maneno ya uongo ndani yake

(vi) Isiwe inaahidi adhabu kali sana kwa kosa dogo sana na isiwe inaahidi malipo makubwa sana kwa amali ndogo.

(vii) Isipinganen na ukweli wa kihistoria

Utangulizi **Alama 01 ½**

Kiini **Hoja 05 @ alama 02 ½ = 12 ½**

Hitimisho **Alama 01**

JUMLA ALAMA 15

11. Qur'an si zao la shaitwani kwa sababu zifuatazo:

(i) Ujumbe wa Qur'an umeteremshwa ili kumtoa mwanadamu kutokana na hadaa zote za shaitwani. Hivyo ingekuwa ni aya za shaitwani asingejidhihirisha kiasi hicho ili watu wamuepuke.

(ii) Qur'an yenyewe imekataa kuwa sio aya za shaitwani. Iweje shaitwani aandike aya zake halafu arudi apinge kuwa sio zake? (Qur'an 81:25)

(iii) Allah (S.W) anasema kama Qur'an ingekuwa inatoka kwa mwingine isingekuwa Yeye bila shyaka tungekuta hitilafu nyingi. Na ukweli ni kuwa Qur'an haina ukinzani.

(iv) Sheitwani anafahamika kuwa ni kiumbe dhaifu, ikiwa ameweza kuleta mazito kama hii Qur'an mbona hapajatokea mashaitwani wengine au wanadamu kujitokeza kuandika mithili yake ili kujibu changamoto iliyotolewa na Qur'an.

Utangulizi **Alama 01 ½**

Kiini **Hoja 4 @ alama 3 = 12**

Hitimisho **alama 01 ½**

JUMLA ALAMA 15

Shulelibrary.com

Shulelibrary.com